| | | |
|---|---|---|
| | JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA<br>**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI** | |

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kwa mujibu wa Ibara ya 75(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ina jukumu la kuchunguza mgawanyo wa Jamhuri ya Muungano katika Majimbo ya Uchaguzi; Tume inaweza kutekeleza jukumu hilo mara kwa mara au angalau kila baada ya miaka kumi.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilifanya Ugawaji wa Majimbo ya Uchaguzi kabla ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 ambapo Majimbo Mapya saba (7) yaliongezwa. Aidha, Tume ilifanya marekebisho ya Mipaka ya Majimbo ya Tanzania Zanzibar kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu 2010, ingawaje idadi ya Majimbo ilibaki kuwa 50.

Kwa kuwa miaka mitano (5) imeshapita na baada ya Serikali kufanya marekebisho ya mipaka ya kiutawala kwa kuanzisha Halmashauri mpya, Tume imefanya zoezi la kuchunguza mgawanyo wa majimbo ya Uchaguzi ya Tanzania Bara kwa ajili ya Uchaguzi wa Wabunge wa mwaka 2015.

Katika kufanya zoezi hili, Tume ilibainisha vigezo vitakavyotumika katika kuchunguza mipaka na kugawa Majimbo ya Uchaguzi. Vigezo vilivyobainishwa ni vile vilivyopo katika Katiba ya Nchi. Vigezo vilivyotumika ni:

1. **Idadi ya Watu,**
2. **Upatikanaji wa Mawasiliano,** na
3. **Hali ya Kijiografia.**

Aidha, mwaka 2010, Tume ilifanya utafiti katika nchi za SADC ili kujua vigezo vingine vinavyotumika katika nchi hizo kwa lengo la kutekeleza jukumu lake la kuchunguza mipaka na kugawa Majimbo kwa ufanisi zaidi.

Baada ya utafiti huo, na kwa kuzingatia mashauriano na Wadau mbalimbali, Tume iliongeza vigezo vingine ambavyo ni:-

1. **Wastani wa Idadi ya Watu (Population Quota),**
2. **Hali ya Kiuchumi,**
3. **Ukubwa wa Eneo la Jimbo husika,**
4. **Mipaka ya Kiutawala,**
5. **Jimbo moja lisiwe ndani ya Wilaya/Halmashauri mbili,**
6. **Kata moja isiwe ndani ya Majimbo Mawili,**
7. **Mpangilio wa Maeneo ya Makazi ya Watu yaliyopo (Existing Pattern of Human Settlement),**
8. **Mazingira ya Muungano,**
9. **Uwezo wa ukumbi wa Bunge,** na
10. **Idadi ya Viti Maalum vya Wanawake.**

Tarehe 28 Aprili, 2015 Tume ilitangaza kuanza kwa mchakato wa ugawaji majimbo kwa Tanzania Bara na mwisho wa kuwasilisha maombi ilikuwa tarehe 30 Mai, 2015.

Katika tangazo hilo, tulibainisha utaratibu uliopaswa kufuatwa na Halmashauri zote katika kuwasilisha maombi/mapendekezo ya kuchunguza Mipaka na kugawa majimbo. Utaratibu ufuatao uliobainishwa:

1. Maombi/mapendekezo ya kuchunguza mipaka na kugawa majimbo yawasilishwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri husika kwa ajili ya kujadiliwa katika vikao rasmi.
2. Baada ya kujadiliwa katika vikao rasmi vya Halmashauri, Mkurugenzi wa Halmashauri husika atawasilisha maombi/mapendekezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa.
3. Katibu Tawala wa Mkoa atawasilisha maombi/mapendekezo katika Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).
4. Baada ya kupitishwa na Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), maombi /mapendekezo hayo yatawasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Vigezo na utaratibu uliotumika upo kwenye Kanuni za Sheria ya Uchaguzi wa Rais na Wabunge za mwaka 2010.

Hivyo, Tume katika kuchunguza na kugawa majimbo imetumia vigezo na utaratibu huo ulioainishwa kwenye kanuni hizo.

Baada ya kupokea maombi/ mapendekezo ya kuanzisha majimbo ya Uchaguzi yafuatayo yamebainishwa:

1. **Jumla ya Halmashauri 37** ziliwasilisha maombi/mapendekezo ya kugawa majimbo ya Uchaguzi.
2. **Majimbo 41** yaliombwa kugawanywa.
3. Baada ya uchambuzi, ni **Majimbo 36 ndiyo yaliyokidhi Vigezo** kwa ajili ya kugawanywa.
4. Kati ya **Majimbo hayo 21 yaliyotokana na kigezo cha mipaka ya kiutawala** yaani Halmashauri mpya zilizoanzishwa na hivyo, kuhitaji Jimbo
5. **Majimbo 15 yametokana na kigezo cha wastani wa idadi ya watu (Population Quota)**.
6. **Majimbo kumi (10) yamependekezwa kubadilishwa majina**.

Ili kuweza kuamua ni majimbo mangapi yaongezwe, Tume ilizingatia Vigezo muhimu vitatu:

1. **Wastani wa Idadi ya Watu (Population Quota).**
2. **Mipaka ya Kiutawala.**
3. **Uwezo wa ukumbi wa Bunge.**

Kabla ya kugawanya na kuanzisha majimbo mapya, Tume ilitembelea majimbo yote yaliyokidhi vigezo na kustahili kugawanya ambapo ilikutana na wadau na kupata maoni yao juu ya jimbo husika.

**Majimbo mapya**

Kwa kuzingatia vigezo vya **Wastani wa Idadi ya Watu (Population Quota), Mipaka ya Kiutawala na Uwezo wa ukumbi wa Bunge** na kwa kuzingatia Ibara ya 75(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ya mwaka 1977, Tume inaanzisha **Majimbo mapya 26** na kukubali **Majimbo kumi kubadilishwa majina**, kwa ufafanuzi ufuatao:

1. M**ajimbo 20 yanaazishwa kutokana na ongezeko la Halmashauri mpya**
2. **Majimbo 6 yanaanzishwa kutokana na kigezo cha wastani wa idadi ya watu (Population Quota)**.
3. **Majimbo kumi yamebadilishwa majina**.

MAJIMBO YALIYOANZISHWA KWA KIGEZO CHA ONGEZEKO LA HALMASHAURI

**Majimbo 20 yanayoanzishwa kutokana na kuanzishwa kwa Halmashauri mpya ni:**

1. Handeni Mjini
2. Nanyamba
3. Makambako
4. Butiama
5. Tarime Mjini
6. Tunduma
7. Nsimbo
8. Kavuu
9. Geita Mjini
10. Mafinga Mjini
11. Kahama Mjini

12. Ushetu

13. Nzega Mjini

14. Kondoa Mjini

15. Newala Mjini

16. Mbulu Mjini

17. Bunda Mjini

18. Ndanda

19. Madaba

20 Mbinga Mjini

**MAJIMBO YALIYOANZISHWA KWA KIGEZO CHA IDADI YA WATU**

**Majimbo 6 yanayoanzishwa kutokana na idadi ya watu ni:**

1. Mbagala – Dar es salaam
2. kibamba – Dar es salaam
3. Vwawa – Mbeya
4. Manonga - Tabora
5. Mlimba - Morogoro
6. Ulyankulu - Tabora

**MAJIMBO YANAYOBADILISHWA JINA**

Majimbo Kumi (10) yamebadilishwa jina

1. **Jimbo la Rungwe Mashariki** Mkoa wa Mbeya**, litaitwa Jimbo la Busekelo**
2. **Jimbo la Rungwe Magharibi** Mkoa wa Mbeya**, litaitwa Jimbo la Rungwe**
3. **Jimbo la Urambo Mashariki** Mkoa wa Tabora, **litaitwa Jimbo la Urambo.**
4. **Jimbo la Urambo Magharibi** Mkoa wa Tabora, **litaitwa Jimbo la Kaliua.**
5. **Jimbo la Njombe Magharibi** Mkoa Njombe, **litaitwa Jimbo la Wanging'ombe**
6. **Jimbo la Njombe Kusini** Mkoa wa Mjombe, **litaitwa Jimbo la Lupembe**
7. **Jimbo la Bariadi Mashariki** Mkoa wa Simiyu, **litaitwa Jimbo la Itilima.**
8. **Jimbo la Bariadi Magharibi** Mkoa wa Simiyu**,** litaitwa **Jimbo la Bariadi.**
9. **Jimbo la Kondoa Kaskazini** Mkoa wa Dodoma, **litaitwa Jimbo la Kondoa.**
10. **Jimbo la Kondoa Kusini** Mkoa wa Dodoma, **litaitwa Jimbo la Chemba.**

**Orodha ya Majimbo yanayoanzishwa kwa ujumla wake**

| S/N | JIMBO JIPYA | HALMASHAURI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 1. | Handeni Mjini | Halmashauri ya Mji Handeni | Tanga |
| 2. | Nanyamba | Halmashauri ya Mji Nanyamba | Mtwara |
| 3. | Makambako | Halmashauri ya Mji Makambako | Njombe |
| 4. | Butiama | Halmashauri ya Wilaya Butiama | Mara |
| 5. | Tarime Mjini | Halmashauri ya Mji Tarime | Mara |
| 6. | Tunduma | Halmashauri ya Mji Tunduma | Mbeya |
| 7. | Nsimbo | Halmashauri ya Wilaya Nsimbo | Katavi |
| 8. | Kavuu | Halmashauri ya Wilaya Mpimbwe | Katavi |
| 9. | Geita Mjini | Halmashauri ya Mji Geita | Geita |
| 10. | Mafinga Mjini | Halmashauri ya Mji Mafinga | Njombe |

| S/N | JIMBO JIPYA | HALMASHAURI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 11. | Kahama Mjini | Halmashauri ya Mji Kahama | Shinyanga |
| 12. | Ushetu | Halmashauri ya Wilaya Ushetu | Shinyanga |
| 13. | Nzega Mjini | Halmashauri ya Mji Nzega | Tabora |
| 14. | Kondoa Mjini | Halmashauri ya Mji Kondoa | Dodoma |
| 15. | Newala Mjini | Halmashauri ya Mji Newala | Mtwara |
| 16. | Mbulu Mjini | Halmashauri ya Mji Mbulu | Arusha |
| 17. | Bunda Mjini | Halmashauri ya Mji Bunda | Mara |
| 18. | Ndanda | Halmashauri ya Wilaya Masasi | Mtwara |
| 19. | Mbagala | Halmashauri ya Manispaa Temeke | Dar es salaam |
| 20. | Vwawa | Halmashauri ya Wilaya Mbozi | Mbeya |
| 21. | Manonga | Halmashauri ya Wilaya Igunga | Tabora |

| S/N | JIMBO JIPYA | HALMASHAURI | MKOA |
|---|---|---|---|
| 22. | Kibamba | Halmashauri ya Manispaa Kinondoni | Dar es salaam |
| 23. | Mlimba | Kilombero | Morogoro |
| 24. | Madaba | Halmashauri ya Wilaya Madaba | Ruvuma |
| 25. | Ulyankulu | Halmashauri ya Wilaya Kaliua | Tabora |
| 26. | Mbinga Mjini | Halmashauri ya Mji Mbinga | Ruvuma |

## Majimbo ya Uchaguzi Zanzibar kwa ajili ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano

Majimbo kwa upande wa Zanzibar yatabaki hamsini (50) kama ilivyo sasa isipokuwa kuna baadhi ya Majimbo Mipaka yake imebadilika na kuongezeka sheia na kubadilika majina. Majimbo hayo ni kama ifuatavyo:-

### Mkoa wa Kaskazini Pemba (Majimbo Tisa)

#### Wilaya ya Micheweni (4)

1. Konde
2. Micheweni
3. Tumbe
4. Wingwi

#### Wilaya ya Wete (5)

5. Gando
6. Kojani
7. Mtambwe
8. Mgogoni
9. Wete

### Mkoa wa Kusini Pemba (9)

#### Wilaya ya Chakechake (5)

10. Chakechake
11. Chonga
12. Ole

13. Wawi
14. Ziwani

**Wilaya ya Mkoani (4)**

15. Chambani
16. Kiwani
17. Mkoani
18. Mtambile

## Mkoa wa Kaskazini Unguja (9)

**Wilaya ya Kaskazini "A"(4)**

19. Chaani
20. Mkwajuni
21. Nungwi
22. Tumbatu
23. Kijini

**Wilaya ya Kaskazini "B" (4)**

24. Bumbwini
25. Donge
26. Kiwengwa
27. Mahonda

Mkoa wa Kusini Unguja

**Wilaya ya Kati (3):**

28. Chwaka
29. Uzini
30. Tunguu

**Wilaya ya Kusini (2):**

31. Makunduchi
32. Paje

**Mkoa wa Mjini Magharibi (22)**

**Wilaya ya Mjini (5):**

33. Amani
34. Chumbuni
35. Jang'ombe
36. Kikwajuni
37. Kwahani
38.Magomeni
39. Mpendae
40. Shaurimoyo
41. Malindi

**Wilaya ya Magharibi"A" (4)**

42. Bububu

43. Mfenesini

44. Mwera

45. Welezo

**Wilaya ya Magharibi "B" (2)**

46. Kiembesamaki

47. Kijitoupele

48. Dimani

49. Fuoni

50. Mwanakwerekwe

**Majimbo yaliyobadilishwa mipaka;**

1. Jimbo la Bububu linaunganisha Bububu, Mtoni na Dole.
2. Jimbo la Mwera linaunganisha Mwera na Mto Pepo.
3. Jimbo la Kiembesamaki linaunganishwa na Chukwani.
4. Jimbo la Kijitoupele linaunganishwa na Pangawe.

**Majimbo yaliyobadilishwa majina**;

1. Mji Mkongwe litaitwa Malindi.
2. Rahaleo litaitwa Kikwajuni.

Hivyo, ongezeko la **Majimbo 26 kwa Tanzania Bara linaongeza majimbo ya Uchaguzi kuwa jumla ya Majimbo 265 Tanzania nzima.**

Jaji wa Rufaa (Mst.) Damiani Z. Lubuva
**MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**